# MAKABURI MAJINI

"Mkazikwa pamoja naye katika ubatizo; na katika huo mkafufuliwa pamoja naye, kwa kuziamini nguvu za Mungu aliyemfufua katika wafu" (Kol.2:12). Katika ubatizo wa Biblia mtu anazikwa katika kaburi la maji na kutoka humo akiwa amefufuliwa kuishi maisha mapya katika Kristo kwa nguvu za Mungu, yaani, Roho Mtakatifu. Hivyo ubatizo una maana yenye kina na ni zaidi ya kuzikwa tu ndani ya maji na kutoka. Unawakilisha kifo, kuzikwa na kufufuka kwa Yesu Kristo.

Paulo anafafanua kwa kusema, "Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi *tuenende katika upya wa uzima*" (Rum.6:4). Wokovu wetu unategemea kifo na kuzikwa na kufufuka kwa Yesu Kristo. Kama hatua zote za awali zimechukuliwa, mtu anayebatizwa anatarajiwa kuendelea kuishi maisha mapya ya ushindi dhidi ya dhambi kwa nguvu ya Roho Mtakatifu.

Ubatizo waweza kuwa ni kwa sababu ya kutimiza haki yote kama Yesu alivyobatizwa katika mto Yordani. Yeye hakuwa na dhambi zo zote kuweza kustahili kubatizwa. "Wakati huo Yesu akaja kutoka Galilaya mpaka Yordani kwa Yohana ili abatizwe. Lakini Yohana alitaka kumzuia, akisema, Mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia, Kubali hivi sasa, kwa kuwa ndivyo itupasavyo *kutimiza haki yote*. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara *akapanda kutoka majini*, na tazama, mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye" (Mt.3:13-17). Ikiwa ubatizo ulikuwa ni wa lazima kwa Yesu ili kutimiza haki yote, je! ni vipi kwetu sisi wenye dhambi?

Kwa kawaida sababu kuu ya kubatizwa ni dhambi. "Ndipo walipomendea Yerusalemu, na Uyahudi wote, na nchi zote za kandokando ya Yordani; naye akawabatiza katika mto wa Yordani; huku wakiziungama dhambi zao" (Mt.3:5). Watu wanaobatizwa wanapaswa ku"zaa matunda yapasayo toba" (Mt.3:8). Vinginevyo ubatizo utakuwa hauna maana kwao maana watakuwa hawajabadilika tabia zao.

Yesu alimwambia Nikodemo, "Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu" (Yn.3:5). Roho anaanza kufanya kazi ndani ya mtu ili kumbadilisha kabla ya ubatizo. Anamwonesha dhambi zake na kumvuta atubu na kumpokea Yesu kwa imani kama Bwana na Mwokozi wake. "Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake" (Yn.1:12). "Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya, ya kale yamepita; tazama! yamekuwa mapya" (2 Kor.5:17).

Hao huzaa matunda yapasayo toba na kuendelea kuishi maisha mapya baada ya kubatizwa. Huenda wengi wanaorudi nyuma baada ya ubatizo hawakupitia hatua hii kabla ya ubatizo wao. Wengine husahau kiapo chao wakati wanapobatizwa. Wengine hawajasalimisha maisha yao kabisa kwa Yesu. Kuna hatua za kufuata kabla ya ubatizo.

"Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa *wanafunzi*, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na *kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru* ninyi; na, tazama, mimi nipo pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari" (Mt.28:19,20). Kabla mtu hajabatizwa sharti la kwanza awe mwanafunzi, afundishwe yote aliyoamuru Yesu na akubali kuyashika yote (kiapo cha ubatizo).

Baada ya kujifunza Neno la Mungu imani inazaliwa ndani yake, anampokea Yesu kama Bwana na Mwokozi wake kwa imani. "Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe, Aaminiye na kubatizwa, ataokoka; asiyeamini,

atahukumiwa”” (Mk.16:15,16). Hatua hizo mbili – kufundishwa na kuamini – ni za lazima kwa kila anayetaka kubatizwa. Mafundisho ya Biblia yako zaidi ya ishirini; mtu akiyaelewa yote atakubali kuishi kwayo kwa nguvu ya Roho Mtakatifu.

Watoto wadogo kwa kuwa hawawezi kufundishwa yote na kwa hiari yao kuamini na kuamua wenyewe kubatizwa, hawabatizwi. Badala yake wanabarikiwa tu. “Basi wakamletea watoto wadogo ili awaguse; wanafunzi wake wakawakemea. Ila Yesu alipoona alichukizwa sana, akawaambia, Waacheni watoto wadogo waje kwangu; msiwazuie; kwa maana watoto kama hawa ufalme wa Mungu ni wao. Amin, nawaambieni, Ye yote asiyeukubali ufalme wa Mungu kama mtoto mdogo hatauingia kabisa. Akawakumbatia, akaweka mikono yake juu yao, ***akawabarikia***” (Mk.10:13-16).

Ukiangalia huku na huku katika ulimwengu wa Kikristo leo unaona kuna ubatizo wa aina nyingi. Wengine wananyunyiza maji mara tatu juu ya kichwa; wengine wanamwagilia maji mara tatu; wengine wanazamisha mwili wote majini. Wengine wanaruka moto, wengine wanapita chini ya bendera na kadhalika. Jambo hili linazusha maswali mengi moyoni. Je, kuna ubatizo wa aina ngapi? Je, mtu akibatizwa kwa ubatizo usiokuwa wenyewe anahesabiwa kama amebatizwa au la? Je, kama ukijulikana ubatizo wa Biblia, hao waliobatizwa kinyume cha huo wabatizwe tena? Wengine wanasema ubatizo wo wote unafaa tu. Wengine wanadai kuwa ni dhambi kubatizwa tena. Ukweli ni upi?

Paulo, muumini wa ubatizo wa kuzikwa majini, anasema, “Mwili [kanisa] mmoja, a Roho mmoja,… tumaini moja… Bwana mmoja, imani moja, ***ubatizo mmoja***. Mungu mmoja…” (Efe.4:4-6). Ingeshangaza sana na kuleta utata mkubwa kama Mungu huyo mmoja angeweka njia mbalimbali za ubatizo. Mwili mzima unazikwa katika kaburi la maji kama alivyozikwa Yesu (Rum.6:4-11; Mt.3:16; Kol.2:12). Mtu aliyezikwa haonekani kwa macho. Amefunikwa kabisa na udongo au na maji. Ubatizo wa kuzamisha unahitaji maji mengi ili mtu anayebatizwa asionekane mwili wake juu (Yn.3:23).

Agano Jipya liliandikwa kwa Kigiriki. Ubatizo ni neno linalotokana na neno la Kigiriki ‘*baptizo*’ limanishalo kuchovya au kuzamisha majini. Kunyunyiza maji kwa Kigiriki ni ‘*rantizo*’. Angesema, Enendeni mkawarantize. Kumwagilia maji kichwani kwa Kigiriki ni ‘*ekchao*’. Angesema, Enendeni mkawaekchae. Hakusema hivyo.

Mtu aliyebatizwa kwa ubatizo wa kuzikwa majini kama hajui mafundisho makuu aliyoamuru Yesu ayashike, atabatizwa tena baada ya kufundishwa (Mdo.19:1-5). Mtu akiasi imani au kurudi nyuma au kutenda tendo linaloliaibisha kanisa katika jumuia, akiondolewa katika ushirika wa kanisa anahesabiwa kama Mmataifa [Mpagani] (Mt.18:15-18; 1 Kor.5:1-5,9-13). Huyo atarudi katika ushirika kwa njia ile ile mpagani anayoingia katika ushirika wa kanisa, yaani, kwa ubatizo. Huo ndio ukweli wa mambo. Hakuna dhambi kufanya hivyo. Kiapo cha ubatizo lazima kijumuishe mambo yote aliyoamuru Yesu, sio machache tu. Anayebatizwa anafungwa na yote.

Ndugu msomaji, kama hujabatizwa ubatizo wa Yesu wa kuzikwa katika kaburi la maji, basi amua kuchukua hatua zote na kula kiapo ili upate kuunganika na Kristo katika kifo, kuzikwa na kufufuka kwake na kuishi maisha mapya katika yeye kwa nguvu za Mungu.

Mfululizo na.15#mm

[TOA FOTOKOPI, UMGAWIE MWENZAKO]